


**YENYI TULISIKIA  
JUU YA:**
**KWA SABABU GANI WANACHANJA WATU WOTE KATIKA ENEO  
KWA SASA. IJAPO KUWA HAIKUFANYIKA MBELE?**

 Fuateni habari za jibu juu ya Ebola  
 katika gazeti ya Radio "Koma  
 Ebola"

 [soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)  
 [Facebook.com/komaebola](https://Facebook.com/komaebola)  
 [@Ebolakoma](https://twitter.com/Ebolakoma)  
 [koma-ebola.info](http://koma-ebola.info)


**TULISIKIA PA  
GOMA**  
 Mwezi wa Kwanza 2020

**MAJIBU**

Wanachanja watu wote katika maeneo zenye zilionesha watu ambao wanahakikishwa kuwa wanganjwa wa ebola. Mbinu ama njia inayoitwa «chanjo kijiografia ya mitaa» inatumikishwa kwa sasa katika maeneo ya afia za Beni, Butembo, Biakato, Aloya, na Bingo - Mabalako.

Hii chanjo inahusu kila mtu (ila tu wanawake wenye kuwa na mimba ya chini ya miezi tatu (3) na watoto wa chini ya miezi sita (6)) ambao wanapatikana katika hizo maeneo za chanjo. Shabaa ya hii mkakati ama ufundi mupya ni kuchanja, kwa muda mfupi, watu wengi ili kukuwa na ukingo wa pamoja ya jamii zidi ya virusi vya Ebola.

Alakini, inashauriwa kuchunguza hatuwa za ukingo hata kama ulipata chanjo.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID). Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.

Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.


Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenye hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana (umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

**YENYI TULISIKIA JUU YA:**

**NINI INAWEZA KUFASIRIYA KESI MPYA ZA UGONJWA KATIKA MIJI KISHA MASIKU BILA KUPATA MUGONJWA?**

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

[soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)  
[Facebook.com/komaebola](https://www.facebook.com/komaebola)  
[@Ebolakoma](https://twitter.com/Ebolakoma)  
[koma-ebola.info](http://koma-ebola.info)



TULISIKIA PA  
**BUTEMBO**  
Mwezi wa Kwanza 2020

**MAJIBU**

Ni kwa sababu watu wamoja hawaheshimiye kanuni za kujikinga na wanakuwa na tabiya ambazo zinahatarisha, alakini pia kuhamishwa kwa watu kwenyi mahali inayo kumbwa na magonjwa nakuenda mahali kwenyi hakuna magonjwa. Inawezekana pia kuna watu wameambukizwa lakini wanajificha, na wamoja wao wanasafiri fasi zingine, na hiyo inahatarisha zaidi kuambukiza watu wengine na kusambaza virusi katika maeneo mengine mapya.

Kwa hiyo ni lazima sana kuheshimia hizo kanuni za kujikinga, na kwenda haraka kwenyi kituo kya afia cha karibu ikiwa kunaonekana dalili au alama za kwanza za magonjwa (kama vile homa, maumivu ya kichwa ...) au kama mtu amegonjwa. Hiyo inasaidiwa kuzuwiya matokeo za mupya wa ebola, inasaidiwa pia kulinda jamii na kuongeza bahati ya kuishi kwa watu.